Historia ya Parokia ya Segerea

Kuanzishwa kwa Parokia

Parokia ya Roho Mtakatifu Segerea iko katika Jimbo kuu la Dar es Salaam. Parokia hii iko katika Manispaa ya Wilaya Ilala chini ya Dekania ya Ukonga. Parokia hii inaendeshwa na wamisionari wafransiskano wakonventuali.

Mapadre watawa wafransisko wakonventuali ni watawa walionzishwa na Mtakatifu Fransisko wa Asizi huko Italia katika karne ya kumi mbili na kwa kuwa ni shirika la kimisionari waliendelea kuenea katika mabara yote. Wamisionari hawa walifika Tanzania mnamo mwaka 1988. Mapadre hawa walianzia kazi zao za kitume katika jimbo la Same katika parokia ya Mwanga na kufikia mwaka 1992 walichukua jukumu la kuhudumia Parokia ya Polising'isi iliyo chini ya Jimbo kuu la Arusha.

Mnamo mwaka 1997 shughuli za kutume zilipanuka zaidi walipoamua kukubali mwaliko wa Mh.Kardinali Polycarp Pengo wa kufanya utume katika Jimbo kuu la Dar es Salaam. Padre Dominiki Wasilewski alikuwa mmisionary wa kwanza wa Shirika la Wafransiskano wakonventuali kuja kuaza kazi ya utume katika jimbo hili.

Kwa kuwa segerea ilikuwa ni kigango kilichokuwa chini ya parokia ya kipawa, padre Dominik alikihudumia chini ya uongozi wa parokia ya kipawa hadi kilipopata hadhi ya kuwa parokia.Padre Domini alianza huduma yake hapa rasmi tarehe 04.01.1998, alipoadhimisha misa kwa mara ya kwanza hapa.
Kufikia mwaka 1998 hitaji la kukipa kigango hiki cha Segerea hadhi ya parokia lilionekana kuwa kubwa. Baada ya makubaliano yaliyofanyika kati ya Wanashirika kuhusu uwezekano wa kuchukua jukumu la kuhudumia kigango hiki, na kupata ruhusa kutoka kwa Provinciali aliyokuwa mhudumu wa shirika katika Jimbo la Warsaw, Jozef Zapinski maandalizi ya kukipatia kigango hadhi ya parokia zilianza.

Uamuzi wa kupata hadhi ya parokia kigango cha Segerea na uliidhinishwa Mh. Kardinali Polycarp Pengo tarehe 29/04/1998. Kwa kipindi chote hiki Padre Dominiki aliishi katika Seminary ya Segerea.



Picha ya Kigango CHA Segerea wakati hu

Maandalizi ya ufunguzi wa parokia mpya yalinza na ujenzi wa nyumba ya mapadre. Shughuli hii ilifanikishwa kwa michango ya waamini wa segerea pamoja na misaada ya wafadhili iliyochangishwa chini ya padre Peter Bijnowski huko Poland.

Ujenzi wa nyumba ya mapadre ulikamilika 1999. Papadre wa kwanza ambao walikuwa ni Padre Dominik Wasileski na Padre George waliweza kunza kuishi katika nyumba mpya ya mapadre tarehe 01/05/1999. Kigango cha kinyerezi kilichokuwa chini ya Parokia ya Ukonga kilifanywa kuwa sehemu ya Parokia hii ya segerea tarehe 04/07/1999.

Kuanza kwa Parokia
Kigango cha segerea kilipewa rasmi hadhi ya Parokia 22/05/1999, kuwa parokia mpya ya Roho mtakatifu Segerea. Mh Kardinali Polycarp Pengo alimteuwa rasmi Padri Dominik Wasileski kuwa Paroko wa Parokia ya Roho Mtakatifu Segerea. Parokia iliendelea kupata huduma chini ya ungozi wa Padre Dominiki na usaidizi wa Padre Peter na Padre George.

Viongozi wa Parokia.
Wahudumu Viongozi wa awali wa parokia hii walikuwa ni ndg.Emanueli Tibaijuka alikuwa mwenyekiti, William Kanaan aliyekuwa mwenyekiti msaidizi, ndugu Credo aliyekuwa katibu na Theresia mbonde aliyekuwa mwenyekiti msaidizi.Viongozi waliofutia ni pamoja na Francis Mgota, Jeremiah Daffa na John Mrema.Kamati ya ujenzi iliundwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kanisa chini ya wajumbe wafuatao:-

Ndg. Prosper Tesha.	Mwenyekiti
Salutaris Masawe	Mwenyekiti Msaidizi
Evarest Ndikilo	Katibu
Fortunatus Kagombora	Katibu Msaidizi
Julius Tibaijuka	Mweka hazina

Washauri

Castor Lumato
Leticia Mosore
Anno Mbilango

Viongozi wa awali wa Kigango.

Costantini Mkinga	Mwenyekiti
Oswald Sokoni	Mwenyekiti Msaidizi
Mama Maria Mtesha	Katekista
Moses Mabindo	Katekista

Kukua kwa Parokia

Baada ya idadi ya waamini kuongezeka ikaonekana haja ya kuboresha miundombinu ya kuabudia na kuwa na kanisa la kisasa. Juhudi zilifanyika kupata wachora ramani (Architects) kwaajili ya ku desgn jengo la kanisa.



Picha ya Parokia ilivyo sasa

Kufuatia ongezeko kubwa la waamini katika parokia ya Segerea,hitaji la kujenga kanisa kubwa zaidi lilionekana kwa kuwa kanisa dogo lililokuwepo lilionekana kutokidhi mahitaji ya wakati ule. Mnamo mwaka 2000 taratibu za mipango ya kukusanya michango kwa ajili ya kanisa jipya ilianza.Padre Peter ambaye alichaguliwa kuchukua kuwa paroko mpya wa parokia hii ya Segerea alianza kazi kama paroko rasmi 19/11/2000.

Mbali na shughuli mbalimbali za ujenzi ambazo ni sehemu ndogo tu ya ukuaji wa parokia,parokia imekuwa zaidi kiroho. Vikundi mbalimbali na vyama vya kutume vimeanzishwa . Mwaka 1999 shirika la utawa wa tatu wa Mt. Fransisco yaani wasekulari lilianza rasmi chini ya uongozi wa ndg Damiani Mkulu kutoka parokia ya Pugu ambaye pia alikuwa mhudumu mkuu wa wasekulari Daresalam. Chama cha vijana rafiki wa mtakatifu Fransisko kilianzishwa pia hapa parokiani.